

Uchanganuzi wa Sitiari za Bahari katika Methali za Waswahili

Sheila Pamela Wandera-Simwa
Chuo Kikuu cha Laikipia

Ikisiri

Makala hii inachanganua sitiari za bahari katika methali za Waswahili. Methali ni mojawapo ya vipera vya fasihi simulizi. Kufuatia ujio wa maandishi na teknolojia, vipera vingi vya fasihi simulizi vilianza kutiwa katika maandishi na kuwa fasihi andishi pia. Kwa mujibu wa Simiyu (2011), ni semi fupi zinazosheheni mafumbo juu ya ukweli wa maisha ya binadamu, naye Mieder (2014) anasema sifa kuu za methali ni ufupi wake, uthabiti na uasili. Fasihi simulizi ya kila jamii huakisi mazingira, utamaduni na mwono-ulimwengu wao. Katika fasihi simulizi zao, mila, desturi na maadili yao pia hujitokeza. Mazingira ya Waswahili yana mchango mkubwa katika kuumba fasihi simulizi yao, methali zikiwemo. Mazingira ya minazi, bahari, vyombo vya bahari, samaki, visima na vitu vingine vinavyopatikana katika mazingira ya Waswahili ndivyo huumba methali zao. Vitu hivi hutumiwa kistiari katika methali zao na kupanua maana za vitu hivyo kifasihi. Makala hii inachanganua sitiari za bahari ambayo ni sehemu mojawapo ya mazingira ya Waswahili.

Maneno Muhimu: Methali, Sitiari, Bahari, Mawanda Chanzi, Mawanda Lengwa, Waswahili.

Utangulizi

Sehemu mojawapo ya mazingira ya Waswahili ni bahari. Bahari imeumba maisha yao. Shughuli za kiuchumi za jamii ya Waswahili hutokana na bahari, na ndiyo hasa kitovu cha uchumi wao. Bahari pia ni mojawapo ya vipengele katika mazingira yao ambavyo vimeunda mwono-ulimwengu, utamaduni na lugha yao. Matumizi yao ya lugha yamesheheni vipengele mbalimbali vya bahari. Jambo hili kwa mujibu wa Lakoff na Johnson (1980) hutokea kwa sababu uhalisia wa maisha ya jamii hueleweka kistiari. Ulimwengu hueleweka kistiari kwa hivyo sitiari zina mchango mkubwa katika uelewa wetu wa mambo mbalimbali ya kidhahania. Kobia (2016) anahoji kuwa sitiari huundwa kutokana na mazingira maalum na ya kawaida ya binadamu. Sitiari hizi hufumbatwa katika fasihi simulizi za jamii mbalimbali kama vile methali, mashairi simulizi na nyimbo.

Mojawapo ya misamiati inayounda lugha inayotumiwa katika methali za Waswahili ni bahari. Uzoefu wao wa bahari umeibua itikadi nyingi zinazoizunguka bahari. Mtagusano wao na bahari umewapelekea kuunda methali ambamo bahari inatumiwa kuwakilisha desturi na mila zao kama zinavyojitokeza katika maisha yao ya kila siku. Methali zao huzipa bahari maana nyingi za kifasihi na maana hizi hupatikana katika sitiari zinazotumiwa katika methali hizo. Methali za Waswahili hutumiwa katika diskosi mbalimbali kwa madhumuni mengi ikiwemo kuadilisha, kuonya, kuhimiza, kutuliza, kuelimisha na kushauri. Emrich (1972) anasema methali hupata umaarufu miongoni mwa wanajamii kwa kuwa huhifadhi utamaduni wao, utambuzi wa kimawazo na tajriba zao za muda mrefu. Kwa hivyo, methali zina umuhimu mkubwa wa kimawasiliano, kuhifadhi utamaduni na zinaweza kuwa kifaa muhimu kinachoweza kusaidia katika kutambua tajriba za jamii lugha na vile inavyouona ulimwengu kwa jumla (Wilson, 2009, Moreno, 2010).

Methali

Methali za Waswahili kama zilivyo methali za jamii nyingine, huakisi mwono-ulimwengu wao ambao ni zao la mazingira yao. Wazo hili linashadidiwa na Monanti na wenzake (2013) wanaposema methali ni mojawapo ya bunilizi za kisimulizi ambazo hutungwa na wanajamii kutokana na mazingira yao. Kila jamii hutenda na kusikiliza bunilizi zao za kisimulizi na hivyo kujenga ulimwengu wao. Mwono-ulimwengu pia huathiri jinsi lugha inavyotumiwa; Kramsch (2008) alihoji kwamba wazungumzaji wa lugha tofauti hufikiri kwa njia tofauti na kuwa na miono-ulimwengu tofauti ya kiutamaduni. Kramsch

(2008) anamaanisha lugha huumba fikra za jamii lugha tofautitofauti, hata hivyo mazingira inamoishi jamii lugha huumba fikra zao pia na kuathiri vile inavyotumia lugha.

Kila jamii ulimwenguni ina methali zake zilizoundwa kutokana na mazingira yao. Methali hizi hueleweka na jamii na huenda mtu wa nje asiyelewa busara na hekima zilizofumbatwa ndani ya methali hizo akakosa kung'amua maana zake. Mara nyingi methali hutumiwa katika mazungumzo ya kawaida baina ya wanajamii kuadilisha, kushauri, kuonya na wakati mwingine kukashifu au kukemea tabia isiyokubalika na jamii. Lewis (1974) anasema methali husimba mfumo wa maadili na matarajio ya jamii kwa wanajamii, hii ina maana kwamba lugha inayotumika huwa ya kimafumbo. Tamathali za usemi ambazo kwa kiasi kikubwa ni mafumbo hujenga methali hizi; Tamathali hizi ni kama vile sitiari, jazanda, kinaya, takriri, chuku, tauria, tashbihi, kejeli na tashihisi.

Misingi ya Nadharia

Makala hii itaongozwa na nadharia ya sitiari tambuzi kwa mujibu wa Kovecses (2010). Nadharia ya sitiari tambuzi iliasisiwa na Lakoff na Johnson (1980) ambao walihoji kuwa sitiari huunda sehemu ya kimsingi katika mfumo wa mawazo yetu. Miongoni mwa wananadharia walioiendeleza nadharia hii ni Gibbs (1994), Dirven na Verspoor (2004), Evans na Green (2006) miongoni mwa wananadharia wengine. Kulingana na Kovecses (2010) kuna aina tatu za sitiari; sitiari za kimuundo, sitiari za kiontolojia na sitiari za mshikamano. Sitiari za bahari zinazopatikana katika methali za Waswahili ni za kimuundo. Sitiari za kimuundo ni zile ambazo husema A ni B; sitiari hizi huhusisha uelewa wa dhana au tajriba fulani na dhana au tajriba tofauti. Kwa ufupi Kovocses (2010) anahoji kuwa sitiari za kimuundo zimekitwa katika tajriba, hivyo hueleweka tu kwa kuzihusisha na mambo ya kitajriba.

Mahusiano ya vipengele katika mawanda chanzi na mawanda lengwa huonyesha tu muundo wa sitiari (Kovecses, 2010). Anaendelea kufafanua kuwa, mawanda hayo mawili huhusishwa pia na tajriba za jamii, mazingira, utamaduni wao na matukio fulani katika jamii hiyo. Kwa hivyo, kwa mujibu wa Kovecses (2010), katika sitiari tambuzi za kimuundo mawanda lengwa hueleweka kutokana na habari zinazojulikana kuhusu mawanda chanzi na tajriba walizo nazo wanajamii katika mawanda hayo. Hili lina maana kuwa ni wazawa wa lugha peke yao na wenyeji wa mazingira husika wanaoweza kuelewa maana ya nyimbo, mashairi au methali za jamii husika ambamo sitiari zimetumiwa. Wazo hilo linashadidiwa na Lakoff na Johnson (1980) wanaposema kwamba sitiari za utambuzi hupenya katika ufahamu wetu wa ulimwengu unaotuzunguka.

Hivyo sitiari huhitilafiana kutoka utamaduni hadi mwingine kwa sababu uundaji wake hutokana na mazingira zinamotungwa. Miundo yake huwa ya kidhahania na isiyoshikika lakini huhusishwa na vipengele vinavyoshikika vilivyo katika mawanda chanzi na kueleweka na jamii-lugha. Kama ilivyo sifa ya sitiari ya kiulinganishi, mawanda chanzi ya sitiari za bahari hulinganishwa na mawanda lengwa kutoka kategoria za kiutambuzi kama vile maadili, wazo, mahusiano ya binadamu na wakati.

Mbinu za Utafiti

Kundi lengwa la utafiti huu ni methali za Waswahili hususan zile ambamo istilahi bahari imetumiwa. Data ilikusanywa kwenye mkusanyiko wa methali 4860 zilizokusanywa na Albert Scheven kati ya miaka ya themanini na tisini. Baadaye zilichapishwa mtandaoni baada ya kifo chake katika mwaka wa 2000. Mbinu ya uteuzi wa sampuli ya kimaksudi ilitumiwa kuteua methali zilizokuwa na sitiari za bahari. Wasailiwa watatu, wenyeji na wakazi wa kisiwa cha Lamu waliteuliwa kimaksudi kuchambua methali teule na kueleza maana kulingana na uelewa wao wa kimazingira ya Uswahilini. Usaili ulifanywa kwa njia ya simu. Mhimili wa kichocheo cha mawanda chanzi na mawanda lengwa wa nadharia ya sitiari tambuzi ulitumiwa kuchanganua sitiari za bahari katika methali nane zilizotafitiwa.

Uchanganuzi wa Methali Teule

Katika makali hii methali nane zilichanganuliwa kwa kutumia nadharia ya sitiari tambuzi kama ilivyokwisha kutajwa na matokeo ni kama yafuatavo:

Avumaye Baharini Papa, kumbe Wengi Wapo

Methali hii imebeba sitiari mbili; bahari na papa, ambazo ndizo mawanda chanzi yanayotumiwa kueleza kuhusu tabia ya majivuno. Tabia ni dhana isiyoshikika lakini hudhihirika katika mienendo ya

mtu. Ni dhana dhahania ya kiutambuzi ambayo huelezeka kiistiari kwa kutumia dhana iliyo katika mawanda chanzi ambayo ina sifa sawa nayo. Kwa mawanda lengwa katika sitiari hii ni tabia. Kamusi ya Kiswahili Sanifu (2013) inafafanua papa kama samaki mkubwa wa baharini mwenye ngozi nene ya kijivu hafifu. Inaendelea kufafanua kuwa wako wa aina nyingi kama vile upanga, pingusi, usingizi na amrani.

Bahari nayo ni eneo kubwa la maji ya chumvi linalozingira mabara na visiwa, sifa ya bahari kuwa na maji ya chumvi inaonyesha dhahiri tofauti kati ya viumbe wanaopatikana humo na viumbe wa majini wanaopatikana katika maziwa na mito. Viumbe wanaopatikana katika maji ya bahari ni wakubwa wakilinganishwa na viumbe wa maji ya maziwani na mitoni.

Sitiari hazichukuliwi tu kama tamathali za usemi zinazojisimamia bali ni ujenzi wa wazo kutokana na tajriba aliyo nayo mtu katika mawanda chanzi hadi mawanda lengwa. Ni aina ya kiungo cha kiakili kati ya dhana mbili zisizo na uhusiano wowote ambayo huruhusu mtu kuwaza na kuzungumza kuhusu dhana dhahania kwa kuzihusisha na sifa za dhana nyingine katika mazingira na kuzua matamshi ya kiistiari yanayohusiana na mawanda hayo (Lakoff 1993 na Evans & Green 2006).

Katika methali ya avumaye baharini papa kumbe wengi wapo sitiari za bahari na papa zinatuwezesha kuzungumza kuhusu tabia ya majivuno kwa kuzitumia kufumbata hisia na mawazo yetu kuhusu tabia hiyo. Charteris-Black (2004) anasema sitiari hutuwezesha kuelewa dhana ngumu, kwamba, ni rasilmali za kimawasiliano ambazo wazungumzaji lugha hutumia ili kufupisha maelezo katika ujumbe wao. Mawanda chanzi ya sitiari hizi ni papa na bahari na mawanda lengwa ni tabia ya kiburi, majigambo na majivuno.

Sitiari	Mawanda Chanzi	Muundo Tambuzi	Mawanda Lengwa
Papa	Mtu mwenye majivuno	Majivuno	Mtu mwenye tabia ya majivuno
Bahari	Ulimwengu	Nguvu	Mali, kimo kikubwa, uwezo

Kwa muktadha wa methali hii bahari inalinganishwa na ulimwengu, vile ulimwengu ulivyo mkubwa, vivyo ndivyo bahari ilivyo kubwa. Imebeba viumbe wa kila aina, mimea, wanyama tofauti na samaki anuwai kila mojawapo ya hivyo viumbe vikiwa na tofauti za kitabia na kimaumbile. Hali hii inapatikana ulimwenguni pia; kwamba ulimwengu umejaa binadamu wanaotofautiana kitabia na kimaumbile. Bahari katika muktadha huu, si ulimwengu tu, inaweza pia kuwa taaluma ambapo mtaalamu mmoja anajiona ndiye mwenye maarifa na ujuzi peke yake kumbe na wapo wengine walio na ujuzi huohuo.

Kitovu cha uchumi wa wenyeji wa pwani mwa Kenya hutokana na bahari. Utalii na uvuvi ndio uti wa mgongo wa uchumi wao. Kwa kuwa wana uzoefu wa shughuli za bahari, wanavijua viumbe vilivyomo na sifa zao. Kulingana nao, samaki wa aina ya papa ndiye mfalme wa Bahari Hindi katika sehemu za Afrika Mashariki. Samaki huyu ana tabia ya kudhalilisha samaki wengine wa baharini, huwashambulia na hata kuwala. Huwashambulia pia binadamu baharini na kuwajeruhi au hata kuwameza. Sifa za papa baharini ni kwamba huvizia na kulishambulia windo lake baharini, hivyo huogopwa sana na binadamu pamoja na samaki wenziwe. Licha ya kuwa ana kimo kikubwa na kuonekana kwamba yeye ndiye anayevuma baharini kwa sababu ya kimo chake na tabia zake zinazozua hofu miongoni mwa binadamu na viumbe wengine wa baharini, siye peke yake aliye na tambo kubwa miongoni mwa viumbe wa baharini.

Kuna samaki wengine kama vile nyangumi, nguru, tengesi, ngisi na jodari ambao ni wakubwa kumliko ilhali hawatii hofu kama anavyofanya yeye. Sitiari ya papa katika methali hiyo inatumiwa kumkashifu mtu mwenye majivuno na kujinaki kwa nguvu alizo nazo au uwezo alio nao, kwamba wapo wengine ulimwenguni wanaomshinda au walio bora zaidi. Mtu aliye na tabia ya kujivuna au kujitapa kwa sababu ya uwezo alionao wa aina yoyote ile hupigiwa methali hii. Mtu wa aina hii akiwa katika eneo fulani ambalo kwa muktadha wa methali hii ni bahari, huvuma, hujulikana sana na kutajika na kwa sababu hiyo kuwadharau watu huku akifikiri kwamba hakuna mwingine aliye na uwezo, ujuzi, mali au hata nguvu alizo nazo, kumbe wengine wapo wala hawajitapi anavyofanya

yeye. Bahari nayo pia ni vivyo hivyo ina samaki wengi wakubwa zaidi kuliko papa walio watulivu na wasiovuma.

Bahari Shwari, haitoi Wanamaji Stadi

Bahari ikiwa shwari haiwezi kuzalisha wanamaji stadi; mtu yeyote anayeogelea katika bahari iliyo shwari hawezi kujifunza mbinu za uogeleaji zinazomwezesha kupambana na ghasia ya bahari. Ni kawaida ya maisha kuwa mtu aliyezoea maisha yasiyo na changamoto yoyote hawezi kuwa na maarifa ya kukabiliana na changamoto za maisha. Maisha ya mtu huimarishwa na changamoto anazopitia maishani. Sitiari zinazojitokeza katika methali hii ni za bahari shwari na wanamaji stadi. Sitiari hizo zimetolewa katika mawanda ya bahari yanayowakilisha maisha na mwanamaji stadi inayowakilisha binadamu vile ilivyoonyeshwa katika jedwali lifuatalo:

Sitiari	Mawanda Chanzi	Muundo Tambuzi	Mawanda Lengwa
Bahari	Changamoto	Changamoto	Maisha
Mwanamaji stadi	Binadamu	Uthabiti	Mtu asiye thabiti katika maisha

Methali hii imezalika katika mazingira ya pwani na inaakisi namna Waswahili wanavyoielewa bahari na kuweza kulinganisha shughuli za baharini na maisha yao ya kila siku. Bahari huchangia pakubwa katika kuumba utamaduni wao, Oyelade (1999) anasema methali ni viashiria vya utamaduni. Viashiria hivyo hueleza mambo mengi kwa maneno machache kuhusu historia na saikolojia ya jamii zinamozaliwa. Wanajamii wanapolelewa katika mazingira fulani hutarajiwa kuwa na ustadi wa kuyamudu mazingira hayo. Kwa mfano, jamii zilizo karibu na bahari, zina idadi kubwa ya wanamaji. Katika mazingira ya misitu, hapana shaka jamii itakuwa na wawindaji wengi.

Bahari shwari ni bahari isiyo na mawimbi, ghasia au mtukutiko, iliyotulia. Bahari shwari haitoi wanamaji stadi ni methali inayodhihirisha uzoefu wa bahari walio nao Waswahili. Wanaifahamu tabia ya bahari kwamba inapokuwa shwari, mwanamaji hapigani na ghasia zinazoweza kuzuka. Kuogelea kwake huwa kwepesi pasi kubuni mbinu mbalimbali za kupambana na mawimbi. Kufuatia hali hiyo, mwanamaji hakuzi ustadi wake wa kuogelea kwa sababu hana msukumo wa kufanya vile. Kupigana na mawimbi baharini ndiko hukuza stadi za mwanamaji. Kadri mwanamaji anapopambana na mawimbi ili kuepuka kuzama ndipo anapokuza stadi zake na kuwa gwiji baharini.

Sitiari zilizo katika methali hii zinalinganisha bahari na maisha, na mwanamaji, na pia binadamu. Mtu huweza kumudu stadi za maisha kupitia kwa changamoto nyingi. Maisha rahisi yasiyo na changamoto zozote humfanya mtu asiwe na ubunifu wowote katika kujikimu kimaisha. Jambo hili humfanya asiweze kukabili changamoto za maisha kwa ustadi. Kwa upande ule mwingine, mtu anayekabiliana na changamoto nyingi maishani huwa na ubunifu katika maisha na kuweza kukabiliana na hali zozote zinazomkabili. Methali hiyo hutumiwa kuwahimiza watu wanaopitia changamoto nyingi maishani kuwa, wajipe moyo kwa sababu changamoto wanazopitia ndizo zitakazoimarisha maisha yao na kuwapa stadi za namna wanavyoweza kujimudu katika maisha. Kwa upande ule mwingine ushwari wa bahari hauwezi kuzalisha mwanamaji stadi; maisha yasiyo na changamoto humdumaza mtu kimaisha.

Mtu halindi Bahari, ipitayo kila Chombo

Kwa mujibu wa Faycel (2012), sitiari husitiri maana nyingi za kistiari. Methali ya mtu halindi bahari ipitayo kila chombo, imesitiri maana zinazoibuliwa kutoka kwa mawanda ya ndoa. Lakoff na Johnson (1980) wanasema mahusiano yanayotokea katika pande zote hujikita kwenye uhusiano wa kistiari na aina hii ya uhusiano hujengeka katika methali kama sitiari za kiisimu. Itikadi, mila, miiko na utamaduni wa Waswahili umejengeka kutokana na bahari na mwono-ulimwengu wao umeumbwa kutokana na tajriba zao za mazingira ya bahari. Methali nyingi zinazorejelea bahari zimebuniwa na zinagusa vipengele mbalimbali vya maisha ya Waswahili. Mtu halindi bahari ipitayo kila chombo ni methali inayohusisha mawanda ya ndoa na bahari pamoja na chombo kama ifuatavyo:

Sitiari	Mawanda Chanzi	Muundo Tambuzi	Mawanda Lengwa
Bahari	Bahari	Ukware	Mwanamke mkware
Chombo	Vyombo vya bahari	Ndoa	Mwanamume anayetaka kuoa

Vyombo vingi kama vile boti, majahazi, madau, mashua, meli, merikebu, manowari na ngalawa hupita baharini. Mawanda chanzi ya bahari yanahusishwa na mwanamake asiyetulia kwa mwanamume mmoja, na mawanda chanzi ya vyombo vya bahari yanahusishwa na wanaume tofautitofauti. Methali hii hutumiwa kama onyo kwa mwanamume anayetaka kuoa mwanamke aliyepotoka kimaadili. Mwanamke aliye na tabia ya kubadilishabadilisha wanaume. Mwanamume huonywa kwa methali hii dhidi ya kumuoa, kwamba hatoweza kumdhambi mwanamke aliyewazoea wanaume tofauti tofauti.

Huwa vigumu kuishi na mwanamke kama huyo kwa sababu amekuwa na wanaume wengi maishani na huenda asiweze kuishi na mmoja pekee. Kwa hivyo, kuna uwezekano kwamba hatatulia katika ndoa; mume hana uwezo wa kuzuia tabia ambazo mwanamke amekua nazo na kuzioea maishani mwake. Itakuwa vigumu sana kumbadilisha mwanamke huyu kitabia. Tajriba za bahari walizo nazo Waswahili zimeunda mwono-ulimwengu wao; kutokana na uzoefu walionao wa bahari wanafahamu tabia ya bahari. Ufahamu huo huibua methali zilizosheheni sitiari ambamo mitazamo yao kuhusu maisha imefumbatwa.

Elimu Bahari, haina Kuta wala Dari

Katika mawanda ya isimu tambuzi, Lakoff na Johnson (1980) wamechangia katika kuasisi sitiari tambuzi ambazo zinapendekeza kuwa ili binadamu waelewe mambo ya dhahania ya kisitiari hutumia kategoria za kimsingi zinazojulikana na tajriba zao wenyewe ili kujenga uhusiano kati ya mawanda. Yu (2014) anasema akili hujenga mawazo kutokana ishara inazopata kutoka kwa mwili unaotagusana na mazingira yetu. Lakoff na Turner (1989) wanasema sitiari tambuzi hutumiwa na jamii yenye utamaduni mmoja. Wanahoji sitiari hizo huwa na utaratibu kwa sababu kuna uhusiano imara kati ya muundo wa mawanda yanayotazamiwa kueleweka na muundo wa mawanda ambayo tayari yanaeleweka. Hii ina maana kuwa, sitiari tambuzi hutokana na mitagusano ya jamii na mazingira yake hivyo kila jamii huwa na sitiari zake tambuzi tofauti na nyingine kwa sababu ya tofauti za mazingira.

Kiasi kikubwa cha methali za Waswahili zimeundwa kutokana na mazingira ya bahari kwa sababu wana tajriba ndefu na mazingira hayo. Methali elimu bahari, haina kuta wala dari inatuleta katika mawanda chanzi ya bahari na mawanda lengwa ya elimu kama inavyoonekana katika jedwali lifuatalo:

Sitiari	Mawanda Chanzi	Muundo Tambuzi	Mawanda Lengwa
Elimu	Bahari	Ujuzi, Maarifa	Masomo, ulimwengu
Kuta	Kuta	Mipaka	Nyumba
Dari	Dari	Nia	Nyumba

Mtu anapompigia mwenziye methali hii, katika utambuzi wake tayari huwa kuna mawanda lengwa ya ujuzi au maarifa; mtu akiwa hai, ataendelea kuelimika katika maisha yake. Mtu akiwa na ari ya kujifunza mambo huwa kama aliye katika safari isiyo na mwisho. Mtu huyo hujifunza mengi kutokana na tajriba zake za maisha, mitagusano na watu mbalimbali na katika taasisi za elimu pia. Bahari haina kuta au kizuizi, maji hupwa na kutamba kwa uhuru. Dari ni sitiari ya nia, mtu akiwa na nia ya kusoma, huwa hana la kukomesha ari yake ya kusoma wala huwa hakuna kuta za kuzuia elimu yake. Kuta ni sitiari ya mipaka, kwamba elimu haina mipaka.

Elimu sio ya darasani tu, haina mipaka inayoitwa shule au darasa. Elimu hupatikana popote, wakati wowote, na wala haina mipaka ya hela. Mtu huweza kuelimika: kutokana na tajriba anazopitia maishani; kutokana na mitagusano na mazingira yake; kutokana na mitagusano na watu mbalimbali katika jamii; na pia, katika taasisi za elimu. Elimu haina mipaka ya umri. Mja huweza kuelimika akiwa na umri wowote ule. Elimu inachukuliwa kuwa kama bahari, kwamba haina kikomo wala

mipaka ya aina yoyote ile. Mradi mtu yuko hai, ataendelea kuelimika maishani. Iwe anapokea elimu yake katika taasisi au nje ya taasisi za elimu, atazidi kuelimika mradi angali hai.

Maji ya Kifuu, Bahari ya Chungu

Inavutia jinsi Waswahili wanavyofungamanisha bahari na dhana nyingine katika mazingira yao kuunda methali. Katika methali ya maji ya kifuu bahari kwa chungu, dhana za chungu na kifuu cha nazi zimetumiwa ili kuonyesha lililo zito kwa mtu mmoja huenda likawa jepesi kwa mwingine. Kwa hivyo, sitiari za bahari, maji na chungu zimetumiwa kama mawanda chanzi kama inavyoonekana katika jedwali lifuatalo:

Sitiari	Mawanda Chanzi	Muundo Tambuzi	Mawanda Lengwa
Maji ya Kifuu	Kifuu kilicho na maji	Changamoto ndogo	Mtu aliye na shida ndogo
Bahari ya chungu	Bahari	Changamoto kubwa	Mtu aliye na shida kubwa

Bahari hutumiwa kistiari na Waswahili katika mawasiliano yao, methali nyingi zimeundwa kutokana na tabia, umbo na mienendo ya bahari kama ionekanavyo machoni mwa Waswahili. Kauli ya Cameron (2010) kwamba sitiari ni fenomena iliyo na sura nyingi inathibitika kwa jinsi Waswahili wanavyohusisha bahari na shughuli, pamoja na hali mbalimbali za maisha yao. Sitiari za kiisimu katika diskosi zinaweza kufunua mambo mengi kuhusu vile watu hufikiria, kuonyesha kaida za jamii kitamaduni au kuonyesha hisia, mitazamo na maadili ya wanajamii. Kwa mujibu wa Kamusi ya Kiswahili Sanifu (2013) kifuu ni ganda tupu na gumu la nazi aghalabu baada ya kukunwa, lenye umbo kama bakuli ndogo. Hii ina maana kwamba kifuu hakina uwezo wa kubeba maji mengi kama yaliyo baharini. Hata hivyo, yanaweza kuwa bahari kwa chungu ambaye ni mdudu ndogo mweusi wa jamii moja na mchwa, siafu na sisimizi.

Maji ya kifuu yasiyoweza kumzamisha mtu au kuleta hasara yoyote yanakuwa bahari kwa chungu. Methali hii hutumiwa katika hali ambayo mtu ana shida ambayo anaiona kuwa kubwa sana na mwingine akaiona ni ndogo. Hali hii hutokea katika maisha hususan kwa mtu ambaye hajawahi kukabiliana na changamoto kubwa katika maisha. Changamoto anayoipitia kwa mara ya kwanza inapomkabili, huiona kuwa kubwa na kufikiri itamshinda. Kinyume na hilo, huwa kuna mtu ambaye tayari amewahi kupitia changamoto hiyo hiyo na kuikabili kwa ushindi; kwake mtu huyu, changamoto hiyo huwa ndogo.

Hali hiyo ndiyo uhalisia mkamilifu wa maisha, kila hatua ya maisha hukumbwa na changamoto zake na mtu anapopitia hatua hizo inaonekana changamoto zake ni ngumu. Kwa wale ambao washapitia changamoto za hatua hiyo, huona ni rahisi wakilinganisha na changamoto wanazopitia katika hatua ya juu zaidi ya maisha. Udogo wa changamoto wanazopitia hulinganishwa na maji ya kifuu ambayo yanaweza kumzamisha chungu kwa sababu ya udogo wake. Hata ingawa huwa machache, chungu huyaona kama bahari. Udogo huo wa chungu hulinganishwa na mtu asiye na maarifa ya kukabiliana na changamoto zake hivyo kila tatizo huonekana kubwa kwake. Methali hii hupigiwa mtu kumhimiza kuwa tatizo analopitia ni dogo sana, na kwamba kuna wengine ambao wamelipitia kabla yake na wakalishinda. Anahimizwa kuwa, bila shaka naye pia atakabiliana na changamoto inayomkabili kwa ushindi.

Bahari haishi Zingo

Sitiari tambuzi sio kipengele cha lugha peke yake ila ni sehemu mojawapo ya kimsingi ya mawazo ya binadamu. Kiasi kikubwa cha lugha ya kisitiari hutokana na ruwaza zilizopo za mawazo ya kisitiari au sitiari tambuzi zinazokuwa katika utambuzi wa msemaji kabla hajatoa matamshi ya kiisimu. Mawanda chanzi ya methali hii ni bahari na hali ya kutangatanga. Jedwali lifuatalo linafafanua muundo wa kisitiari wa methali hiyo.

Sitiari	Mawanda Chanzi	Muundo Tambuzi	Mawanda Lengwa
Bahari	Bahari	Changamoto	Ulimwengu, Maisha
Zingo	Machafuko au ghasia za bahari	Matatizo, changamoto, mashaka	Changamoto

Mazingira ni mojawapo ya vipengele vinavyosaidia kuumba utamaduni wa jamii pamoja na mwono-ulimwengu wao (Yu, 2014). Matamshi ya kiisimu ya jamii hutokana na sitiari zilizojikita katika utambuzi wao. Lugha ambayo wanajamii hutumia huwa na viashiria vya utamaduni na mazingira yao na mambo wasiyoweza kueleza kwa sababu ni ya kidhahania, huelezwa kisitiari kwa kuhusisha mawanda dhahania yasiyoshikika katika utambuzi wao lakini yaliyo na sifa sawia na mawanda walio na uzoefu nayo; mawanda yanayoshikika. Kwa kuhusisha vipengele katika mawanda chanzi na vipengele katika mawanda lengwa, wanajamii huweza kuibua maana zinazoeleweka katika mazungumzo yao.

Neno bahari limetumiwa kisiari katika methali hii kwa maana ya ulimwengu. Bahari ni kubwa na mambo mengi hufanyika mle; huwameza waogeleaji, vyombo huzama na machafuko huweza kutokea na kusababisha uharibifu usiokadirika. Kwa hivyo, matatizo mbalimbali huwakabili walio baharini kama yanavyokabili ulimwengu. Katika muktadha wa methali hii, ulimwengu unaweza kuwa dunia au maisha katika ulimwengu. Dunia inaweza kubadilika kutokana na hali ya joto, tabia ya nchi, mtetemeko wa ardhi na mambo mengine yanayodhibiti uhai katika sayari ya ulimwengu. Mambo hayo hutokea mara kwa mara na kubadilisha jioografia ya dunia. Mabadiliko hayo hayaishi na huzua matatizo mengi duniani kama vile mitetemeko ya ardhi, mafuriko yanayosababisha hasara kuu, kiangazi kinachoangamiza viumbe-hai, na mifugo pamoja na binadamu duniani, kusababisha majangwa. Vile vile, sitiari ya bahari katika methali hii inahusishwa pia na maisha ya humu ulimwenguni; kwamba yana changamoto zisizo na kikomo.

Kwa kuwa Waswahili wana tajriba ndefu ya tabia za bahari, inakuwa rahisi kwao kuelewa maisha yalivyo kwa kuyahusisha na bahari. Bahari haishi machafuko au ghasia, hivyo hivyo maisha hayaishi changamoto, matatizo, shida au mashaka. Kama bahari, maisha pia yana tabia ya kutanga, hayana utulivu wowote. Maisha ni sawia na bahari, hayana utulivu wowote. Kila hatua ya maisha ya binadamu huja na changamoto kwa hivyo matatizo, mashaka na masumbuko hayaishi katika maisha ya mtu. Akikabiliana na changamoto moja, nyingine inazuka kwa sura tofauti. Ndipo wakasema Waswahili kuwa bahari haishi zingo. Kwa maneno mengine, maisha au dunia haishi changamoto. Methali hiyo hupigiwa watu ili kuwahimiza wasikate tamaa kwa kuwa ndiyo hali ya ulimwengu na maisha kwa jumla.

Fuata Mto, uone Bahari

Miji ya Waswahili iko katika pwani ya Afrika Mashariki na visiwa vyake ambavyo vimo ndani ya Bahari Hindi (Wandera 1996). Baadhi ya mito kutoka bara humwaga maji yake ndani ya bahari; kwa mfano mito Goshi, Tiwi, Pemba, Uмба, Athi, Tana, Ramisi na mingineyo. Maji ya mito ni machache yakilinganishwa na maji ya bahari, isitoshe mito ina kina kifupi ikilinganishwa na bahari. Mito iliyotajwa ikifuatwa kutoka chanzo chake hadi inapoishia, itaishia baharini; methali hii inatokana na hali hiyo. Hata hivyo, sitiari zilizomo zinaashiria mambo tofauti kama yanavyojitokeza katika jedwali lifuatalo:

Sitiari	Mawanda Chanzi	Muundo Tambuzi	Mawanda Lengwa
Mto	Mto	Ishara, bidii	Ishara ndogo ndogo zinazoweza kujenga ushahidi, Bidii
Bahari	Bahari	Chanzo na mwisho wa jambo, ufanisi	Ukweli wa jambo, Mafanikio maishani

Methali hii ina mawanda chanzi mawili, mto na bahari. Hata ingawa ina mawanda lengwa mawili kwa kila mawanda chanzi, mawanda lengwa ya ishara na bidii yanahusishwa na mawanda chanzi ya mto ingawa kitendo cha kufuata ndicho kinaibua maana iliyojitokeza. Inaweza kupigiwa mtu akiambiwa atie bidii kidogo kidogo katika lolote analofanya na mwishowe atapata kufanikiwa; lile dogo aliloanza nalo litakuja kuwa kubwa. Mawanda lengwa ya ukweli wa mambo na mafanikio maishani yanahusishwa na bahari. Fuata mto uone bahari ni methali inayopigiwa mtu anayehimizwa kupeleleza jambo kwa kufuata ishara zitakazomwelekeza kwa ukweli kuhusu jambo analopeleleza. Kwamba hawezi kupuza mambo madogomadogo yanayojenga lile kubwa kama vile bahari

inavyojengwa na mito. Ili mtu kufanikiwa maishani, huanzia chini kabisa na polepole anajijenga hadi anafanikiwa pakubwa maishani.

Bahari iliko, ndiko Mito iendako

Mito mingi huwa na chanzo milimani na midomo baharini, maziwani au katika mito mingine.

Methali bahari iliko ndiko mito iendako inaakisi ukweli wa kauli hiyo. Hata hivyo maneno bahari na mito yametumiwa kistiari katika methali hii. Bahari ni mojawapo ya mazingira ya Waswahili na kutokana na tajriba na ufahamu walio nao wa bahari, fasihi simulizi zao huakisi mazingira yao. Kovecses (2010) anashadidia kauli hizo anaposema kuwa sitiari za kiutambuzi hutokana na michakato ya mahusiano inayofanyika katika utambuzi. Mahusiano haya hufanyika kati ya mawanda chanzi na mawanda lengwa kama invyodhihirika katika jedwali lifuatalo:

Sitiari	Mawanda Chanzi	Muundo Tambuzi	Mawanda Lengwa
Bahari	Bahari	Umoja, utajiri, uamuzi	Watu wengi, Utajiri
Mto	Mto	Muongano, uamuzi	Watu wachache, umasikini

Mawanda chanzi ya methali hii ni bahari na mto. Kijiografia, midomo ya mito ni bahari, maziwa na wakati mwingine mito. Mto ni mdogo ukilinganishwa na bahari, kwa muktadha wa methali, mito huenda bahari iliko. Jambo linaloshadidiwa na wengi huwalazimu wachache wanalolipinga kukubaliana nalo. Waswahili huitumia methali hii wanapohimiza umoja na uamuzi wa jambo kwa pamoja miongoni mwao. Pamoja na methali hii kuleta maana ya umoja katika uamuzi wa mambo, inaonyesha pia kuwa pesa huenda kule ambako tayari kuna pesa nyingine. Kwa maneno mengine watu walio na pesa hutangamana wenyewe kwa wenyewe. Watu hufuata utajiri, aliye na pesa hakosi marafiki. Kwa hivyo, sitiari ya bahari katika methali hii ina maana ya uamuzi wa wengi na utajiri.

Hitimisho

Kama ilivyotajwa awali, tajriba, mazingira na utamaduni wa binadamu huumba mwono-ulimwengu wake. Methali huakisi maadili, imani na mila za jamii. Ni hifadhi muhimu ya utamaduni wa jamii. Matamshi ya kiisimu ya methali ni ya kistiari na hutokana na mahusiano ya dhana kati ya mawanda chanzi na mawanda lengwa. Makala hii imechunguza sitiari za bahari katika methali nane za Waswahili ili kubaini matumizi yake katika methali. Imebainika dhahiri kwamba hutumiwa kwa maana tofautitofauti. Kwa mfano, katika methali avumaye baharini papa kumbe wengine wapo, sitiari ya bahari inaashiria mali, tambo kubwa na uwezo. Katika methali ya bahari shwari haitoi wanamaji stadi, sitiari ya bahari ina maana ya maisha. Katika methali, ya bahari iliko ndiko mito iendako sitiari ya bahari ina maana ya uamuzi wa wengi na utajiri.

Elimu bahari haina kuta wala dari ina sitiari ya bahari ambayo inaleta maana ya maarifa au ujuzi ambao mtu huendelea kujifunza maishani pasi kikomo. Katika methali ya maji ya kifuu bahari kwa chungu, sitiari ya bahari imetumiwa kwa maana ya changamoto au matatizo ya maisha. Sitiari ya bahari katika methali ya mtu halindi bahari ipitayo kila chombo, ina maana ya mwanamke mkware. Methali ya bahari haishi zingo ina sitiari ya bahari ambayo ina maana ya ulimwengu na maisha. Methali ya mwisho ni ya fuata mto uone bahari ambapo sitiari ya bahari ina maana ya mafanikio au ukweli wa jambo.

Methali nyingine ambazo zina sitiari za bahari ni kama vile maji meupe baharini, lakini pwani hayanishi nyota, bahari hailindwi, mchelea bahari si msafiri na bahari haivukwi kwa kuogelea. Zipo methali nyingine zilizo na viashiria vya bahari ingawa haziitaji moja kwa moja kama vile mbwa hafi maji akiona ufukwe, dau dogo huwambaa mwambao, kubwa huenda kwenye kilindi, na penye mawimbi na milango ipapo. Kimsingi sitiari za bahari katika methali za Waswahili zinalifanya neno bahari kuwa na maana mbalimbali kifasihi. Maana ya bahari imepanuliwa kifasihi katika methali zao na kubeba maana zifuatazo: maisha, maarifa, ujuzi, mwanamke mkware, taaluma na shughuli mbalimbali, changamoto za maisha, ulimwengu na mafanikio kama zilivyojitokeza katika methali zilizochunguzwa.

Marejeleo

- Cameron, Lynne. (2010). "What is Metaphor and Why does it Matter?" In Cameron, L. R. Masleneds.), *Metaphor Analysis. Research Practice in Applied Linguistics, Social Sciences and the Humanities*, 3-25. London and Oakville: Equinox.
- Charteris-Black, J. (2004). *Corpus Approach to Critical Metaphor Analysis*. Basingstoke: Palgrave.
- Claire Kramsch (2008) "Language, Thought, and Culture." In Alan Davies and Catherine Elder (eds). *The Handbook of Applied Linguistics*, Pp 138-159.
- Dirven, R., & Verspoor, M. (eds.). (2004). *Cognitive Exploration of Language and Linguistics* (Vol. 1). John Benjamins Publishing.
- Emrich, D. (1972). *Folklore on the American land*. Little Brown and Company.
- Evans, V. & Green, M. (2006). *Cognitive Linguistics: An Introduction*. London: Routledge
- Faycel, D. (2012). "Food Metaphors in Tunisian Arabic Proverbs." *Rice Working Papers in Linguistics* 3/1.
- Gibbs, R. W. (1994). *The Poetics of Mind: Figurative Thought, Language, and Understanding*. Cambridge University Press.
- Joseph, J. E. (1996). "The Immediate Sources of the Sapir-Whorf Hypothesis." *Historiographia Linguistica* 23, 365-404.
- Kamusi ya Kiswahili Sanifu*. (2013). Chuo Kikuu cha Dar es Salaam: TATAKI.
- Kobia, J. M. (2016). A Conceptual Metaphorical Analysis of Swahili Proverbs with Reference to Chicken Metaphor. *International Journal of Education and Research*, 4(2), 217- 228.
- Kövecses, Z. (2002). Cognitive-Linguistic Comments on Metaphor Identification. *Language and Literature*, 11(1), 74-78.
- _____ (2010). *Metaphor: A Practical Introduction*. Oxford University Press.
- Lakoff, G. and Johnson, M. (1980). *Metaphors We Live By*. University of Chicago Press.
- Lakoff, G., & Turner, M. (1989) *More than Cool Reason: A Field Guide to Poetic Metaphor*. Chicago: University of Chicago Press.
- Lakoff, George. (1993). "The Contemporary Theory of Metaphor." In Ortony, A. (ed.), *Metaphor and Thought*, 202-251. Cambridge: Cambridge University Press.
- Lewis, Mary Ellen B. "The Feminists Have Done It: Applied Folklore." *Journal of American Folklore*, Vol. 87, No. 343, 1974. Print.
- Mieder, W. (2014). *Behold the Proverbs of a People: Proverbial Wisdom in Culture, Literature, and Politics*. University Press of Mississippi.
- Monanti, N., Okong'o, J. B., Amayi, Z. na Wafula, R. (2013). "Oral Poetry for Enviromental Conservation: A Study of Selected Gusii Texts." In *Journal of Emerging Trends in Educational Research and Policy Studies (JETERAPS)* 5(1): 25- 34.
- Moreno, A. I. (2010). An Analysis of the Cognitive Dimension of Proverbs in English and Spanish: The Conceptual Power of Language Reflecting Popular Beliefs. *SKASE Journal of Theoretical Linguistics*, 2(1):42-54.
- Oyelade, Aderemi Raji. (1999). "Post Proverbials in Yoruba Culture: A Playful Blasphemy." *Research in African Literatures*. Vol 30, No. 1 Pp74- 82. Indiana University Press.
- Simiyu, Fred Wanjala. (2011). *Kitovu cha Fasibi Simulizi*. Mwanza: Serengeti Educational Publishers Ltd
- Wilson, F. C. (2009). *A Model for Translating Metaphors in Proverbs (French to English): A Cognitive Descriptive Approach*. Ph.D. Thesis, University of British Columbia (Okanagan).
- Wandera, S.P. (1996). Usawiri wa mwanamke katika Ushairi wa Kiswahili: 1800-1900: Uhalisi au ugandamizwaji? Tasnifu ya M.A. Chuo Kikuu cha Egerton.
- Yu, Ning. (2014). "Embodiment, Culture and Language." In F. Sharifian (Ed), *The Routledge Handbook of Language and Culture*. Abingdon, Great Britain: Routledge.

